HabariLeo Jumapili Juni 28, 2026 Pg 5.

# Mabasi ya mwendokasi, daladala kutumika Sabasaba

Na Ikunda Erick

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeruhusu Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na daladala kutoa huduma maalumu za usafiri kwenda na kutoka Viwanja vya Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu 'Sabasaba'.

Hatua hiyo imelenga kukidhi ongezeko la mahitaji ya usafiri wakati wa maonesho hayo ya kimataifa yanayoanza leo hadi Julai 13, mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa Latra, Salum Pazzy mamlaka hiyo ilisema mabasi yote yatakayoshiriki kutoa huduma hiyo ni lazima yawe na leseni hai ya usafirishaji na yatoze nauli kwa kuzingatia viwango elekezi vilivyowekwa na Latra.

Aidha, Latra imeelekeza kuwa safari zianzie na kuishia katika vituo vilivyoainishwa kwenye leseni za mabasi husika. Kwa mfano, daladala ya Tegeta Nyuki–Makumbusho inaweza kuendelea hadi Sabasaba na baadaye kurejea Makumbusho kuchukua abiria wanaorejea Tegeta Nyuki.

Mamlaka hiyo pia imewataka madereva kuzingatia sheria na kanuni za leseni ya usafirishaji pamoja na sheria ya usalama barabarani, ikiwemo kutopakia au kushusha abiria katika maeneo yasiyo vituo rasmi na kufuata maelekezo yatakayotolewa ndani ya viwanja vya maonesho ili kupunguza msongamano.

Vilevile, madereva na makondakta wametakiwa kuvaa sare safi na nadhifu pamoja na kutumia lugha ya staha kwa abiria.

Kwa upande wa daladala zinazopita kwenye barabara zilizo sambamba na miundombinu ya BRT ya Morogoro na Kilwa, Latra imeeleza kuwa hazitaruhusiwa kupakia wala kushusha abiria hadi zitakapofika kwenye barabara ambazo si sambamba na njia hizo.

Kwa mabasi yaendayo haraka, Latra imezitaka kuhakikisha zinaweka utaratibu utakaorahisisha upatikanaji wa tiketi kwa abiria wanaokwenda na kutoka katika Maonesho ya Sabasaba, ili kuboresha utoaji wa huduma kipindi chote cha maonesho.

CS CamScanner